**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI**

**Mkoa wa arusha**
**Barua zote ziandikwe kwa:**
**Simu na:**
**Mkuu wa shule +255 764 961 311**
**Makamu mkuu wa shule +255 759 682 793**

**ENGUTOTO SEKONDARI**
**S. L. P 143**
**MONDULI**

**Unapojibu tafadhali taja:**
**KUMB. NA: ENG/SS/F5. JOING./2023/01**
**NDUGU MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………………….**
**SHULE ATOKAYO……………………………………………**

**SHULE YA SEKONDARI ENGUTOTO**

**S.L.P142**

**MONDULI**

**12.06.2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ENGUTOTO HALMASHAURI YA MONDULI MKOA ARUSHA MWAKA 2023**

**1.** Ndugu Mzazi/Mlezi Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya HGL/HKLkatika shule ya sekondari ENGUTOTO. Nitumie nafasi hii, kukupongeza wewe na mwanao kwa kupata bahati hii, ambayo watu wengi wameikosa. **HONGERA KWA KUCHAGULIWA NA KARIBU SANA** katika shule ya sekondari **ENGUTOTO** kwa ajili ya kupata **ELIMU**

**BORA**. Ni matumaini yangu kuwa, mwanao ataitumia nafasi hii vizuri kwa manufaa yake binafsi, familia na Taifa kwa ujumla.

Shule ya sekondari ENGUTOTO, ipo mjini MONDULI mkabala na kituo cha Mafuta GAPCO, ambacho pia ni kituo cha Mabasi maarufu kwa jina la "SHELI" kilichopo katika barabara kuu ya ARUSHA ~ MONDULI. Shule ya sekondari Engutoto, ni ya **BWENI** kwa kidato cha **1** hadi cha **6**. ( Wavulana tu). **Shule itafunguliwa rasmi tarehe 13/08/2023** na **mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/08/2023**. Mwanafunzi anatakiwa afike siku hiyo kabla ya saa 10:00 jioni bila kukosa, akiwa ameambatana na Fomu zote zilizoambatanishwa na barua hii, zikiwa zimejazwa kikamilifu na wahusika na kuzikabidhi shuleni wakati wa usajili.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

I. Suruali 2 za heshima rangi ya kahawia zenye marinda.

**II.** Shati 3 za heshima rangi nyeupe **mikono mirefu,**

III. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi; **SIO BUTI**

IV. Suruari mbili za heshima rangi ya kijivu kwaajili ya kuvaa siku ya kwenda msikitini au kanisani.

V. Soksi jozi tatu rangi nyeusi ,

VI. Mkanda mweusi wa kawaida usio na urembo.

VII. Sweta rangi nyeusi yenye ufito mweupe shingoni na mikononi.

**VIII.** Jezi za michezo rangi ya **blu bahari**

IX. Tracksut rangi ya **blu bahari**

X. Tai rangi ya kahawia.

XI. Shuka mbili za rangi ya kijani

XII. Blanketi moja

XIII. Ndoo mbili za maji

XIV. Mto mmoja

XV. Sanduku la Bati

XVI. Neti ya kuzuia mbu

XVII. Tshirt rangi blue bahari

***N.B. MARUFUKU KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI.***

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iii. Scientific Calculator; kwa wanafunzi wa tahusi ya HGL
iv. Godoro la futi tatu.
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) vya bati sio plastic. Ni MARUFUKU kwa mwanafunzi yeyote Kuchangia vyombo wakati wa kula
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
x. Madaftari makubwa 7 Counter book quire 3
xi. Madaftari madogo 7
xii. Mkebe “mathematical set”
xiii. Kamusi ya kingereza (oxford/Longman dictionary)
xiv. Kalamu za kutosha, rula na pensel
xv. Mfuko (school bag) mzuri na imara kwa ajili ya kubebea vitabu na daftari za shule
xvi. Sanduku la Bati
xvii. Neti ya kuzuia mb
xviii. Tshs 6000/= kwa ajili ya kukata Bima ya afya
**xix. VITABU**

- Kila mwanafunzi aje na vitabu vya mchepuo wake kwa kila somo kama ifuatavyo

**GEOGRAPHY**

- Advanced level practical geography by zisti Kamili
- Human and economic geography by Msabila D.T
- Physical geography by Pritchard

**ENGLISH LANGUAGE**

- Advanced level English by Asheli Nicholaus
- Advance level literature by Nyambari. N.& Bukabile

**KISWAHILI**

- Nadharia ya fasihi by **Kilangi E Lucas,** tahakiki ya kiswahili by kilangi
- Kiwsahili 1 shule za sekondari kidato cha 5&6.
- Riwaya nuta ni kuvute, kufikirika, mfadhili, nguzo mama, kivuli kinasihi morani
- Nadharia ya fasihi by Nyamabri N. & g. Bukagile

**HISTORY**

- World history by **Idrissa Msuya** au Contemporary historical events advanced level history history 1&2 By Shibital C.K

**GENERAL STUDIES**

- Understanding advanced level general studies by Bigirwamungu J. AND Deogratius S.M

## 2.3 Michango mbalimbali

### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Ndugu Mzazi/Mlezi, Jumla ya Fedha yote unayopaswa kumlipia mwanao ni Tshs 80,000/=kwa mwaka au Tshs 40,000/=kwa muhula wa kwanza. Ili aweze kusajiliwa Fedha hiyo ilipwe katika Tawi lolote la Benki ya NMB kabla mwanafunzi hajaripoti shuleni. Jina la Akaunti ni “ENGUTOTO SECONDARY SCHOOL COLLECTION “ Namba ya Akaunti ni 41301100040.

Mwanafunzi atakaporipoti shuleni, ni lazima awasilishe nakala ya BANK PAY-IN SLIP (BPS), ikionyesha wazi, jina kamili la mwanafunzi huyo na sio jina la

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia

mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 3. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**
**FORM A**

**PART A**

ENGUTOTO SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 143
TEL: +255 764 961311, 0759 682 793 MONDULI
15.06.2023
REF.NO:ENG/SS/F.V.JOING/2023.

TO: THE MEDICAL OFFICER,
……………………………….
………………………………

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO:**
**Mr. ………………………………………………………… FORM 5~ 2023**

v. **Please** examine the above named as to his physical and mental fitness for full time schooling course. The Examination should include the following categories [i-iii].

vi.

vii. (i) (a) Eye

viii. (b) Hearing

ix. (c) Limbs

x. (d) Speech

xi. (e) Venereal disease (s)

xii. (f) Leprosy

xiii. (g) Epilepsy

xiv. (ii). Neuroses

xv. (iii)Other serious diseases

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI ENGUTOTO**
**TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI**
**FOMU B**

**SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE KWA HERUFI KUBWA:**

1. (i) JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………
NB: Jina liwe lile lililotumika katika mtihani wa kidato cha nne - 2022.
(ii) Tarehe ya kuzaliwa ………………… kijiji …………………… kata ……………
Tarafa ……………………….. Wilaya ……………………….. Mkoa……………
(iii) Dini ………………………………………… Madhehebu ……………………….
2. AFYA:
(i) Taja magonjwa yoyote makubwa uliyowahi kuugua k.m.f. TB, POLIO, KIFAFA n.k.
…………………………………………………………………………………………
(ii) Taja matatizo yoyote ya afya yako ……………………………………………..
3. JINA LA MZAZI/MLEZI:
(i) Baba ………………………………………… Hai/ Amefariki Lini …………....
(ii) Mama ………………… Hai/ Amefariki Lini ……………….( Kata isiyostahili)
4. KAZI YA:
(i) Baba ……………………Dini ………………… Madhehebu …........................
(ii) Mama …………………..Dini …………………. Madhehebu …………………
(iii) Anwani ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………….....
(iv) Mwanafunzi anaishi na: (Weka V sehemu iliyo sahihi)
(a) Baba tu (b) Mama tu (c) Wazazi wote wawili (d) Mlezi
5. MZAZI/MLEZI/TAASISI ITAYOGHARAMIKIA MAHITAJI YA SHULE:
(i) Jina ……………………………………………………………………….
(ii) Kazi yake ni ……………………………………………………………………
(iii) Anuani yake ni …………………………..... (iv) Simu ……………………………..
(v) Uhusiano wake ………………………. (Mf. Baba, Mama, Dada, Mjomba n.k)
(iv) Dini yake …………………………..... Madhehebu ……………………………….

**6. UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI:**

Mimi ……………………………….. nakubali kujiunga na Shule ya ENGUTOTO Sekondari na kuthibitisha kuwa, nitafuata sheria na taratibu zote za Shule hii ili nitimize lengo la kuja shuleni kwa manufaa yangu/ familia na Taifa kwa ujumla.

Endapo nitakwenda kinyume na Sheria /Kanuni /Taratibu za shule nitakubali kuadhibiwa kulingana na sheria.


Saini ya mwanafunzi ………………………………. Tarehe …………………………….

**7. SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI/MLEZI/TAASISI HUSIKA:**

Mimi ……………………………………. Nathibitisha kuwa, taarifa hiyo hapo juu ni sahihi. Ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule na walimu wote kuhakikisha kijana wangu anakuwa na NIDHAMU na JUHUDI katika masomo. Aidha, nitagharamia Mahitaji yake ya shule, ili kumjengea mazingira mazuri ya kusoma katika kipindi chote atakachokuwa shuleni kwa kuzingatia sheria/ Kanuni na Taratibu za Shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi/Taasisi ……………………………….. Tarehe ……………

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**




**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0764 961 311**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0759 682 793**
- **Mwandamizi Taaluma 0685 888 852**
- **Mwandamizi Malezi 0682 130 892**